**OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA NKASI**


**SHULE YA SEKONDARI NKASI**
**S.L.P 119,**
**NAMANYERE-NKASI**
**11/12/2020**


**JINA LA MWANAFUNZI:**________________________________________________

**S.L.P** ________________

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI NKASI MWAKA 2021**

Ninafurahi kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na **Shule ya Sekondari Nkasi** kidato cha kwanza mwaka 2021. Shule ipo umbali wa km 2 kutoka makao makuu wa wilaya ya Nkasi (Namanyere).

Muhula wa kwanza wa masomo utaanza tarehe **11/01/2021.** Hivyo unatakiwa kuripoti tarehe **11/01/2021** bila kukosa.

**<u>MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA</u>**

**A) SARE YA SHULE (WASICHANA)**

- Sketi moja nyeusi, na moja rangi damu ya mzee kitambaa kizito (sketi ndefu ya kisasa)
- Shati mbili nyeupe mikono mifupi
- Soksi nyeupe pea mbili
- Viatu vyeusi soli fupi pea mbili (viatu vya kamba)
- Vifaa vya michezo (tishet ya bluu, raba)
- Sweta rangi ya bluu
- Tisheti za shule zinapatikana shuleni

**B) SARE YA SHULE (WAVULANA)**

- Suruali mbili nyeusi na damu ya mzee kitambaa kizito (isiwe ya kubana au modo)
- Shati mbili nyeupe mikono mifupi

- Soksi nyeusi pea mbili
- Viatu vyeusi soli fupi vya kufunga kamba visivyo vya mchongoko pea mbili
- Vifaa vya michezo (Tisheti ya bluu, bukta ya bluu na raba)
- Sweta rangi ya bluu
- Tisheti za shule zinapatikana shuleni

**NB:** Kwa waislamu rangi ya hijabu iwe nyeupe

**C) VIFAA VYA KITAALUMA**

i) Daftari za kutosha saizi kubwa (counter book) kuanzia 9
ii) Biki za kutosha
iii) Mkebe mpya wenye vifaa vyote
iv) Kamusi/Dictionary kwa ajili ya Kiswahili/kiingereza

**D) SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na.25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na.10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara ya Elimu na mafunzo ya ufundi yenye dhamana ya elimu nchini na ofisi ya Rais TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala mara baada ya kuripoti shuleni.

a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi, wanafunzi na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima
c) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa
d) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hivyo wakati wote wa wanafunzi wako katika shule hii.
e) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
f) Kuvaa sare wakati wote unapotakiwa
g) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote
h) Kutunza mali za umma

**E) MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA SHULE**

1. Wizi
2. Uasherati na ushoga
3. Ubakaji
4. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi cocaine, mirungi na kubeli na kadhalika.
5. Kupigana au kupiga
6. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
7. Kudharau bendera ya Taifa
8. Kuwa mjamzito/kupata mimba/kumpa msichana ujauzito

9. Kutoa mimba
10. Kugoma kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvunga amani na usalama wa shule au watu.
11. Kukataa adhabu kwa makusudi
12. kuwa na simu ya mkononi
13. Kukutwa au kuonekana kwenye baa au kumbi za sterehe
14. Utoro

**F) MAMBO MENGINE YANAYOPASWA KUKAMILISHWA NA KUWASILISHWA SHULENI NA MWANAFUNZI**

a) Medical Examination form ambayo itajazwa na mganga mkuu wa hospitali ya serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa mkuu wa shule mara utakaporipoti shuleni.
b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.
c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine ya shule.

NB: Fomu za afya na mikataba vitarejeshwa shuleni mwanafunzi anapokuja kuripoti.

Pia mwanafunzi anaporipoti lazima aje na cheti cha kuzaliwa(Birth certificate)

Tafadhali zingatia maelekezo yote uliyopewa katika fomu hii ili kuepusha usumbufu usio wa lazima.

Ninakutakia maandalizi mema na ninakukaribisha sana Nkasi Sekondari.

## FOMU YA MKATABA KATI YA MZAZI KWA AJILI YA KUJIUNGA NA SHULE SEKONDARI NKASI

**A) MWANAFUNZI**

Mimi ________________________________________ninakubali/sikubali kujiunga na shule ya sekondari Nkasi na kwamba nitasoma mpaka kidato cha nne. Aidha niko tayari kufuata sheria kanuni na taratibu zote za shule. Pia nimesoma maelekezo na maagizo yote ya kujiunga na shule na nitatekeleza.

**SAHIHI YA MWANAFUNZI**________________________________

**B) MZAZI/MLEZI**

Mimi______________________________________________________Mzazi/mlezi wa_______________________________________________ ninakubali mwanangu asome shule ya sekondari Nkasi na nitamsimamia mwanangu kuzifuata taratibu zote za shule. Pia nikotayari kutekeleza maagizo na maelekezo yote ya kujiunga na shule ya sekondari Nkasi

**SAHIHI YA MZAZI/MLEZI** ____________________________________

## (C) FOMU YA MKATABA WA KUTOSHIRIKI MIGOMO, FUJO NA MAKOSA YA JINAI SHULENI

Mimi ________________________________________ mtoto wa ____________________________ wa kijiji cha ____________________ ninaapa kuwa nitasoma kwa bidii hadi kuhitimu kidato cha nne, sitaacha shule, sitashiriki mgomo wowote, fujo yoyote shuleni, sitaharibu mali ya shule kwa makusudi na wala sitajihusisha na makosa ya jinai.

Endapo nitafanya moja kati ya mambo hayo juu, hatua kali za kisheria zichukuliwe dhidi yangu ikiwa ni pamoja na kufukuzwa shule au kufungwa jera.

Sahihi ________________________ Tarehe_______________________

***(fomu hii ijazwe na irudishwe shuleni)***




**AMIANIE JOHN MANGA**
**MKUU WA SHULE**
**0756781097/0756502216**